**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Malaysia**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

**Toleo Na: HTM 1447 / 11** | **Jumatano, 17 Dhu al-Hijjah 1447 H** | **03/06/2026 M**


## Taarifa kwa Vyombo vya Habari

## “KL Headline Msimu wa 2026”: Serikali ya Madani Haijali tena Ghadhabu ya Mwenyezi Mungu!

**(Imetafsiriwa)**

Kuala Lumpur iko tayari kuibuka kama mahali mwanana pa ziara za matamasha ya kimataifa barani Asia kupitia “KL Headline Msimu wa 2026,” ambao unakutanisha maonyesho 25 ya wasanii wa kimataifa katika mwaka mzima wa 2026. Mji mkuu wa Malaysia umepangwa kuwa mwenyeji wa maonyesho 25 ya wasanii wa kimataifa katika maeneo sita, yakiwalenga zaidi ya mashabiki 500,000 kutoka pwani za ndani na nje ya nchi - kulingana na mratibu, Live Nation Malaysia. “Msimu wa KL Headline unatarajiwa kushuhudia maelfu ya raia wakichukua fursa hiyo kupata tikiti za matamasha na maonyesho makubwa zaidi ya mwaka,” alisema Waziri wa Mawasiliano, Fahmi Fadzil, wakati wa hotuba yake katika uzinduzi wake mnamo Mei 25, 2026.

Tamasha la Maji na Muziki lililokashifiwa vikali limepita hivi karibuni, na kusababisha Serikali ya Madani kujaribu “kusafisha” Bukit Bintang kwa visomo vya Quran na programu za Swala katika juhudi za kutuliza hasira za Waislamu. Sasa, serikali hiyo hiyo kwa fahari inachafua Kuala Lumpur tena, si kwa “najisi” mmoja (Rijs), bali kwa “najisi kubwa” (Al-Rijs al-Mughallazah) 25. Huu ndio uhalisia wa ufisadi uliomo katika mfumo wa kidemokrasia wa kibepari wa leo, uliotokana na itikadi ya kisekula, ambayo hunyanyua burudani hadi kuwa kitu “cha lazima” kulingana na mtindo wa maisha wa anasa ambao hutumika kama nguzo yake ya msingi.

Mfumo wa kidemokrasia, uliotokana na fikra ya ubepari, ni mfumo ambao haujishughulishi kamwe na mipaka ya Halal (yanayoruhusiwa) na Haram (yaliyokatazwa), kwani jambo pekee linalozingatiwa kwa hatua yoyote ni manufaa ya kimada. Kwa msingi huu, milango ya uovu huachwa wazi katika mfumo huu wa kikafiri, maadamu shughuli hizo za dhambi zinaleta faida. Ili kuzidisha mambo, vitendo vyovyote vya Haram vinavyofanywa na serikali, ikiwa havitakabiliwa na ukimya, “husafishwa” na Mufti na mamlaka za kidini ambao hupokea mishahara minono kutoka kwa serikali. Kwa hivyo, serikali sio tu haijutii majuto bali pia inajivunia makosa makubwa yanayofanywa nao.

Ingawa nchi hii imekumbwa na majanga mbalimbali yanayosababishwa na mikono michafu ya watawala wake, wanaendelea kupuuza maonyo haya maadamu mazao yake ya kifedha yanabaki yamejaa. Ghadhabu ya Mwenyezi Mungu (swt) haizingatiwi kamwe katika hesabu zao, kwani lengo lao kuu ni juu ya faida za kidunia pekee. Watawala hawa, ambao wanapaswa kutumika kama ngao ya Ummah dhidi ya moto wa Jahannam, badala yake hufanya kama mawakala wanaoutumbukiza Ummah kwenye shimo la uharibifu. Huku wakitangaza nchi hii kuwa mfuasi sugu wa mafundisho ya Ahlu Sunnah Wal Jamaah, wakati huo huo wanaandaa matamasha mengi ya dhambi ambayo yanapingana waziwazi na Sunnah!

Kinachosikitisha zaidi na cha kukatisha tamaa ni kwamba kuwa mwenyeji wa Msimu wa KL Headline 2026 kunatokea huku Gaza ikiwa bado imejaa damu, ikionyesha kwamba serikali hii imepoteza hisia yote kwa hali mbaya huko Gaza. Inawezekanaje kwamba huku Gaza ikichinjwa mchana na usiku, Malaysia inashiriki katika sherehe kubwa?! Kwa kweli, wakati serikali hii haiogopi tena ghadhabu ya Mwenyezi Mungu (swt), kimsingi imepoteza kila kitu - hisia, heshima, hisia ya aibu, uchamungu, na achilia mbali hamu ya Jihad Fi Sabilillah. Kwa kualika ghadhabu ya Mwenyezi Mungu (swt) kimakusudi mara kwa mara, hakuna kilichobaki cha serikali hii isipokuwa uovu.

**Enyi Waislamu!** Suala lisilokwisha la burudani kupita kiasi katika nchi hii halijitokezi katika ombwe; badala yake, linatokana na mfumo na mtindo wa maisha ulioingizwa kutoka Magharibi, ulioundwa kufisidi na kudhoofisha umma wa Kiislamu, na muhimu zaidi, kuwatenga Waislamu na imani yao. Matamasha haya ya uovu ni moja tu ya matunda yaliyooza kutoka kwa mti wenye sumu wa demokrasia, uliopandwa katika ardhi za Waislamu na Magharibi. Watawala wa Waislamu, tangu zamani hadi sasa, wamekuwa ndio wanaounyunyizia maji, kuutunza, na kuulinda mti huu wenye sumu. Umma wa Kiislamu lazima uelewe kwamba hadi mti huu ung'olewe kabisa, utaendelea kuzaa matunda yenye sumu ambayo yataharibu yeyote anayeyala.

**Ewe Serikali ya Madani!** Tunatoa pingamizi yetu kali kwa Msimu wa KL Headline 2026. Tunakuhimiza na kukukumbusha kufuta matamasha yote ya uovu ambayo umepanga na kuidhinisha, kwani matendo yako yanatumika tu kukaribisha ghadhabu ya Mwenyezi Mungu (swt). Kumbuka kwamba nchi hii si mali yako binafsi kufanya nayo upendavyo. Nchi hii ni ya Ummah wa Kiislamu, na ardhi hii ni ya Mwenyezi Mungu (swt), iliyokabidhiwa kwako kutawala kulingana na mapenzi Yake, si kulingana na matamanio yako maovu. Kwa kukaribisha ghadhabu ya Mwenyezi Mungu (swt), kwa kweli unakaribisha adhabu Yake. Unaweza kufurahia kwa muda mfupi katika ulimwengu huu na Msimu wako wa KL Headline, lakini adhabu kali na ndefu inakungojea Akhera.

**Ee Mwenyezi Mungu, Mola wetu Mlezi!** Ibadilishe haraka serikali hii inayokuasi na kuwapotosha wanadamu kutoka kwenye njia Yako, kwa utawala wa Kiislamu chini ya Khilafah Rashida kwa njia ya Utume. Ameen Ya Rabbal Alameen.

**Abdul Hakim Othman**
**Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir**
**Malaysia**